

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**RC MAKONDA AREJESHA NYUMBA ZILIZOPIGWA MNADA NA BANK
IKIWEMO YA MAMA MJANE.**

Mkuu wa mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda leo amekabidhi hati ya nyumba kwa familia ya Bi. Zainabu Kaswaka iliyoteseka na kusababisha ugonjwa wa Kupooza kwa Mume wake baada ya nyumba na ardhi yao kuuzwa baada ya Matapeli kutumia hati ya nyumba yao kuchukuwa mkopo Benki ya FNB pasipo familia kujua.

Upatikanaji wa hati hiyo umekuja baada ya majadiliano ya kina baina ya RC Makonda, Wanasheria na Bank ya FNB iliyotoa Mkopo ambapo baada ya Mkuu wa mkoa kuagiza kufanyika uchunguzi ambapo Benki ilibaini uzembe wa baadhi ya watumishi wao wa Benki hiyo uliophelekea kasoro hiyo.

RC Makonda pia amefanikiwa kumuhakikishia makazi ya kudumu Mama Mjane Bi. Benadetha Rwendera alietakiwa kuondoka kwenye nyumba yake na kujikuta akilala nje baada ya kununua eneo na kujenga nyumba pasipokujua kuwa aliemuuzia eneo tayari alikuwa amechukuwa Mkopo Bank ya KCB jambo lililophelekea nyumba kuvunjwa na kuuzwa ambapo baada ya majadiliano baina ya RC Makonda na Bank ya KCB walifiki kwa pamoja kumuachia mjane aendelee kuishi wakati kesi ikiendelea mahakamani na pindi hukumu itakapotoka utafanyika mgawanyo wa ardhi.

Aidha RC Makonda amesema hadi sasa Mkoa umefanikiwa kusikiliza kesi za Wananchi zaidi ya 1,028,000 ambapo Kesi zilizotatuliwa ofisini kwake ni 628,000 na kesi zilizokwenda mahakamani ni 60 ambapo Kati ya hizo kesi 17 zameshatolewa hukumu na watu kupata haki zao chini ya usimamizi wa Ofisi

ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kupitia msaada wa Mawakili waliowasimamia bila malipo.

Itakumbukwa RC Makonda aliahidi kuwasaidia wananchi wasiokuwa na uwezo wa kulipa mawakili Bure na haya Ndio matunda yake.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

25/06/2018